Maswali

1. Pauli alienda mji gani alipotoka Athene?
2. Paulo alifanya urafiki na nani alipokuwa Korintho?
3. Paulo, Akila na Prisila walifanya kazi gani kila siku?
4. Walifanya nini mpaka usiku?
5. Wayahudi waliaamini Injili?
6. Paulo alisema badala yao atahubiria wakina nani Injili?
7. Mungu aliambia Paulo nini kwa ndoto
8. Paulo aliishi muda gani Korintho akihubiri Injili?
9. Mbona Wayahudi walikasirikia Paulo?
10. Wayahudi walitaka kuadhibu Paulo namna gani? Nini kilitendeka?

Majibu

1. Paulo alienda Korintho.
2. Paulo alikuwa rafiki wa Prisila na Akila.
3. Walihubiri Injili kila siku.
4. Walitengeneza mahema kutoka kwa manyoya ya mbuzi. Walizungumza juu ya neno la Mungu.
5. Hapana. Wayahudi hawakuamini Injli.
6. Paulo alisema, badala yao atahubiria Mataifa.
7. “Usiogope. Sitaacha mtu yeyote akudhuru. Wengi wa Wakorintho wataamini Injili.”
8. Paulo alikaa Korintho kwa mwaka moja na nusu.
9. Paulo alihubiria Mataifa. Wayahudi hawakupenda watu wa Mataifa. Wayahudi hawakufikiria kwamba watu wa Mataifa wanaweza kuokoka.
10. Wayahudi walipeleka Paulo kotini aende aadhibiwe. Galio hakukuwa na haja. Wayahudi walipiga Sosthene mkuu wa sinagogi. Galio hakuwajali.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2

98 Paulo akiwa Korintho

Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 18 : 1 – 17

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo alifanya kazi kila siku akihubiri Injili kwa bidii.

Somo

Paulo alipotoka Athene alienda Korintho. Korintho ilikuwa bandari kando ya pwani. Ulikuwa ndiyo mji mkuu wa kusini ya Yunani. Korintho ulikuwa mji wa biashara kubwa. Watu wengi kutoka nchi tofauti walikuja huko kununua na kuuza. Huo mji ulikuwa na uovu mwingi sana.

Paulo alipokuwa Korintho, alifanya urafiki na Myahudi mmoja jina lake Akila na mkewe Prisila. Kazi yao ilikuwa kutengeneza mahema. Hiyo ndiyo ilikuwa kazi yao tu.

Paulo alipokuwa mdogo aliishi Tarso. Tarso ilijulikana kuwa na manyoya ya mbuzi. Mahema ya Bedui yalitengenezwa kutoka kwa manyoya ya mbuzi. Babaye Paulo alimfundishwa kutengeneza mahema ya manyoya ya mbuzi. Paulo alikuwa mtengenezaji wa mahema kama Akila na Prisila.



Prisila na Akila walisaidia Paulo kuhubiri Injili kila siku. Tena walifanya kazi usiku kucha wakitengeneza mahema. Walipokuwa wakifanya kazi walizungumzia neno la Mungu.

Paulo alihubiria Wayahudi Injili kwa Sinagogi. Aliwambia kwamba Yesu ni mwokozi tulioahidiwa na Mungu. Yesu alikufa msalabani lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu.



Wayahudi hawakuamini Paulo. Walikasirika sana. Walimpigia kelele na kumgemea.

Mungu alikuwa amemchagua Paulo ahubirie Mataifa Injili. Wayahudi hawakutaka kusikiliza Paulo. Paulo aliambia Wayahudi, “Damu yenu iwe juu ya vichwa vyenu! Kutoka leo nitaenda kuhubiri kwa Mataifa.”

Paulo alienda kuishi kwa nyumba iliyokuwa karibu na Sinagogi. Paulo alikuwa na mikutano mingi kwa nyumba yake. Alihubiri Injili kwa yeyote aliyependa. Krispo mkuu wa Sinagogi aliamini. Krispo pamoja na familia yake waliamini na wakabatizwa. Watu wengi wengine waliamini na wakabatizwa. Wayahudi walikasirika sana. Walimchukia Paulo.

Wayahudi walimchukia Paulo sana. Wayahudi wa miji mingine walikuwa wamejaribu kuua Paulo. Kama Paulo angeendelea kukaa Korintho, uhai wake ulikuwa hatarini.

Usiku moja Paulo akawa na ndoto. Mungu akamwambia, “Usiogope. Endelea kuhubiri. Niko pamoja nawe. Hakuna atakayekushambulia au kukuumiza. Nitakuweka salama. Kuna watu wengi hapa Korintho watakaokuamini.”

Mungu alimpa Paulo moyo, kwa sababu alimwahidi kumlinda. Paulo aliwahubiria Wakorintho kila siku.

Wayahudi walikasirika sana. Mungu alikuwa amewaita Wayahudi wawe watu wake wateule. Hawakuamini kwamba watu Wamataifa wanaweza kuokoka. Waliwachukia watu Wamataifa. Hawangeweza kula nao wala kuingia kwa nyumba yao. Paulo alikuwa anahubiria Mataifa. Paulo aliambia kila mtu kwamba Mataifa wataokolewa kupitia kwa Yesu. Hii ilikasirisha Wayahudi zaidi.

Kwa pamoja, Wayahudi walipanga kumnyamazisha Paulo. Walimshika Paulo na kumpeleka kotini. Galio alikuwa amekaa kwa kiti cha hukumu. Wayahudi waliambia Galio, “Huyu mtu anaambia watu waabudu Mungu kwa njia isio haki.” Walitaka Galio aadhibu Paulo na amueke gerezani. Galio hakushugulika na shida za Wayahudi. Aliwafukuza.

Galio hangeweza kuadhibu Paulo. Kadhalika Wayahudi hawakujaribu kumuumiza Paulo. Hii ilikasirisha Wayahudi zaidi. Walimshika Sosthene, aliyekuwa mkuu wa Sinagogi yao mgeni. Walimpiga yeye badala ya Paulo. Wayahudi walipiga Sosthene mbele ya Galio. Lakini Galio hakujali.

Mungu alimlinda Paulo. Paulo alikaa Korintho mwaka moja na nusu akihubiri Injili. Watu wengi waliamini na wakabatizwa. Paulo alianzisha eklesia (kanisa) kubwa Korintho. Baadaye Paulo aliandikia eklesia ya Koritho barua tatu au nne. Baadhi ya hizo barua tunazo mbili katika Agano Jipya.